

Mhe, Mwenyekiti,

Kamati ya uchumi inajumuisha idara tano nazo ni idara ya mifugo na uvuvi, idara ya kilimo, umwagiliaji na ushirika, idara ya ujenzi, idara ya ardhi pamoja na idara ya Mazingira.

Mhe, Mwenyekiti

Kamati ya uchumi ilikaa kikao chake mnamo tarehe 13.04.2017 na kisha kuazimia yafuatayo;

- Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kupitia ofisi ya ardhi iwafidie wamiliki wa ardhi ili Wah. Madiwani pamoja na wananchi wengine waweze kumiliki viwanja vyao walivyoununua pamoja na kuendelea na shughuli zingine.
- Afisa kilimo na ushirika aangalie na kufuatilia mali zote za ushirika ambazo zipo mikononi mwa watu ikiwa ni pamoja na kujua kuwa zipo ngapi, na ni za aina gani, kinanani wanamiliki mali hizo.

Mhe, Mwenyekiti

Naomba Baraza lako tukufu liweze kuridhia mapendekezo na maazimio yaliyoafikia na kamati.

Nawasilisha.

.....

Richard Maponda

MWENYEKITI KAMATI YA UCHUMI